

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA AROBAINI NA NANE**

**18 JUNI, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**KIKAO CHA AROBAINI NA NANE TAREHE 18 JUNI, 2024**

**I. DUA:**

**II. TAARIFA YA SPIKA:**

**III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

#### **IV. MASWALI:**

##### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

##### **614. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali inaratibu vipi Miradi inayozinduliwa na Mwenge.

##### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **615. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ahadi ya kurekebisha Barabara za Mji wa Karatu Km 10 itatekelezwa.

##### **616. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Barabara za Mbogwe Vijijini ambazo hazipitiki kabisa.

**617. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapandisha hadhi Shule ya Sekondari Igurubi kuwa ya Kidato cha Tano na Sita.

**618. MHESHIMIWA ROSE CYPRIAN TWEVE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Halmashauri ngapi zimetekeleza agizo la Waziri Mkuu kununua dawa za Viuadudu kutoka Kiwanda cha Kibaha ili kutokomeza mazalia ya Mbu.

**WIZARA YA NISHATI:**

**619. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-



Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na matatizo ya *Low voltage* katika Mji wa Mafinga unaokuwa kwa kasi kwa viwanda na makazi.

**620. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuongeza kasi ya Wakandarasi wa umeme Jimboni Busanda ili wakamilishe kwa wakati.

**WIZARA YA UJENZI:**

**621. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Karavati na kuweka kifusi Barabara inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Njombe kupitia Luteba.

**622. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itanza ujenzi wa Barabara ya Handeni – Mziha – Turiani kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**623. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwainua Wajasiriamali wadogo kufikia Uchumi wa Viwanda.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**624. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, kuna mpango gani wa kusaidia Mradi wa ufugaji Samaki katika Shamba la Samaki JKT Kilombero linalozalisha Samaki 90,000 badala ya 500,000.

**625. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI  
(TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itajenga Mnada wa Mifugo wa Magena ili Wananchi waweze kuuza Mifugo yao.

**WIZARA YA MADINI:**

**626. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA  
(URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, ni Madini aina gani yanapatikana katika Wilaya ya Urambo na Wananchi wananufaikaje na Madini hayo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**627. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS  
(IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itatoa Vitambulisho vya Taifa katika Kata 11 za Jimbo la Igalula.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **628. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, nini mkakati wa Serikali katika kuimarisha kilimo cha Alizeti na Ufuta katika Mkoa wa Songwe.

#### **V. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

#### **WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
18 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**